# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)

# KANUNI ZA KATIBA YA CHAMA ZA MWAKA 2006

## Rekebisho la Pili 2016

# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)

# KANUNI ZA KATIBA YA CHAMA ZA MWAKA 2006

## REKEBISHO LA PILI - 2016

# TUICO
# KANUNI ZA KATIBA YA CHAMA 2006

Rekebisho la Kwanza 2011

Rekebisho la Pili 2016

# YALIYOMO

Ukurasa


1. Jina na Imani ............ 5
2. Anuani ya Chama ............ 5
3. Misingi Mikuu ya Chama ............ 6
4. Shughuli Kuu za Chama ............ 6
5. Lengo la Utekelezaji wa Shughuli za Chama ............ 7
6. Uanachama ............ 7
7. Huduma kwa Wanachama ............ 8
8. Huduma kwa Mwanachama ambaye ajira yake imekoma .... 8
9. Uanachama wa Heshima ............ 9
10. Ushiriki wa Wanachama wa Makundi Maalumu katika Chama 9
11. Ofisi za Chama ............ 10
12. Utendaji wa Ofisi ............ 10
13. Sekta, Idara na Vitengo ............ 11
14. Matawi, Mikoa, Kanda na Taifa ............ 12
15. Vikao vya Chama ............ 16
16. Uendeshaji wa Vikao vya Chama ............ 16
17. Uchaguzi Mkuu wa Chama ............ 17
18. Kugombea Uongozi katika Chama na sifa zake ............ 18
19. Viongozi na Watendaji wa Chama ............ 19
20. Kusimamishwa kwa muda haki ya kupiga/kupigiwa kura..... 19
21. Wajumbe wa Mikutano Mikuu ya Uchaguzi wanaomaliza muda wao wa Uongozi ............ 20
22. Maandalizi na Usimamizi wa Uchaguzi ............ 21

23. Mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama ............ 22
24. Matukio yasiyotarajiwa kabla ya Uchaguzi........................ 23
25. Kujaza nafasi za Uongozi zilizowazi ................................ 24
26. Nafasi za kuteuliwa katika Chama ................................ 26
27. Waalikwa kwenye vikao vya Baraza Kuu ......................... 26
28. Mapato ya Chama ........................................................ 27
29. Fedha na Mali za Chama ............................................ 28
30. Malipo ya Viongozi na Watendaji ................................... 28
31. Mfuko Maalumu wa Akiba/ Mgomo ................................ 28
32. Uwezo wa Chama kukopa ............................................ 29
33. Usimamizi wa fedha za Chama Tawini ............................ 29
34. Ukaguzi wa fedha, mali na daftari la Wanachama ............ 30
35. Ushirikiano na Asasi za Kijamii .................................... 31
36. Kuvunjwa au kuunganishwa Vyama ................................ 31
37. Mgogoro kati ya TUICO na Chama Shiriki cha Shirikisho.... 31
38. Utumishi ndani ya Chama ............................................ 32
39. Sekretarieti ya Chama ................................................ 32
40. Ajira za Mikataba ya Muda Maalumu ............................ 32
41. Miiko, Maadili na Mamlaka ya Udhibiti ............................ 33
42. Washauri wa Chama.................................................... 34
43. Wahamasishaji wa Chama............................................ 35
44. Majadiliano na Migogoro ya Kikazi ................................ 35
45. Mgongano wa Tafsiri na Matumizi ya Kanuni ................... 35
46. Utaratibu wa Hati ya Idhini ............................................ 36
47. Marekebisho ya Kanuni za Chama ................................ 36

# KANUNI ZA KATIBA YA CHAMA

*Kanuni hizi zimetungwa na kuandikwa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya 2004, Kifungu cha 47, na kwa kuzingatia Katiba na matakwa ya Wanachama wenyewe kwa ajili ya maendeleo yao na umoja wao. Kanuni hizi zitasomeka pamoja na Katiba ya Chama na Kanuni nyingine za Chama zilizopitishwa na Baraza Kuu.*

## 1. JINA LA CHAMA

Jina la Chama litakuwa **TANZANIA UNION OF INDUSTRIAL AND COMMERCIAL WORKERS;** kwa kifupi **"TUICO" (CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI).**

TUICO ni Chama huru cha Wafanyakazi kwa ajili ya Wafanyakazi ambacho shughuli zake kuu ni kuhakikisha kuwa kinasimama katika misingi mikuu ya Vyama vya Wafanyakazi na kutekeleza madhumuni ya uwepo wake kwa Wanachama. Hivyo rasilimali za Chama zitaelekezwa katika kuhakikisha shughuli kuu za Chama zinatimizwa na wala si kujipatia kipato au faida.

## 2. ANUANI YA CHAMA

TUICO Makao Makuu,

Mtaa wa Shariff Shamba Ilala,

Kiwanja Na.21 "Kitalu C",

S.L.P 5680, Dar es Salaam.

Barua pepe: tuico2004@yahoo.com

## 3. MISINGI MIKUU YA CHAMA

Misingi Mikuu ya Chama ni hii ifuatayo:-

(i) Uhuru na Demokrasia.

(ii) Umoja na Mshikamano.

(iii) Utawala wa Sheria.

(iv) Haki na Wajibu.

(v) Usawa na Heshima.

(vi) Nidhamu na Uwajibikaji.

(vii) Mahusiano mema.

## 4. SHUGHULI KUU ZA CHAMA

Katika kuzingatia misingi na kutekeleza madhumuni ya Chama na Mpango Mkakati shughuli zifuatazo za Ujenzi na Uimarishaji wa Chama zitafanyika:-

(i) Kuhamasisha na kuingiza Wanachama.

(ii) Kutoa elimu na mafunzo.

(iii) Kukusanya na kusimamia mapato ya Chama.

(iv) Kujadili na kufunga Mikataba ya Pamoja.

(v) Kuunda Kamati mbalimbali za Chama.

(vi) Utetezi na uwakilishi wa Wanachama.

(vii) Kuendeleza Mahusiano na wadau wengine ndani na nje ya nchi.

## 5. LENGO LA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI NA MISINGI YA CHAMA

Utekelezaji wa shughuli na Misingi ya Chama ina lengo la kumwezesha Mfanyakazi:-

(a) Kustawi kiuchumi.

(b) Kuwa salama katika ajira, afya na maisha yake.

(c) Kuheshimiwa na kutambuliwa utu wake.

(d) Kuwajibika na kupata haki zake.

(e) Kushiriki na kushirikishwa katika shughuli za Chama.

(f) Kuwa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi.

(g) Kuwa mbunifu katika kuboresha maisha yake kiuchumi na kijamii.

(h) Kuwa Mwanachama mweledi na rasilimali bora kwa Chama, Wanachama wenzake na jamii.

## 6. UANACHAMA

(a) Mfanyakazi yeyote aliyeajiriwa katika Sekta za Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri na shughuli nyingine zinazohusiana nazo, anayo haki ya kuwa Mwanachama wa TUICO.

(b) Mfanyakazi anayejitegemea mwenyewe/aliyejiajiri atakuwa na haki ya kuwa Mwanachama, pia atakuwa na haki ya kuungana na Wanachama wenzake katika vikundi vya ajira na kuanzisha Matawi ya Mseto.

## 7. HUDUMA KWA MWANACHAMA

(i) Mwanachama yeyote mbali na Wanachama wa Heshima, atagharamiwa na Chama katika utetezi dhidi ya Mwajiri wake kwa mashitaka ya kikazi dhidi yake.

(ii) Mwanachama ambaye ni mjumbe anayehudhuria Vikao vya Uchaguzi na vikao vingine vya Kikatiba, atagharamiwa na Chama kwa mujibu wa Taratibu na Kanuni za Chama.

(iii) Kwa kuzingatia Taratibu na Kanuni za Chama, Mwanachama atafaidika na mipango ya elimu na mafunzo yatolewayo na kugharamiwa na Chama.

## 8. HUDUMA KWA MWANACHAMA AMBAYE AJIRA YAKE IMEKOMA

Mwanachama ambaye ajira yake imekoma na taarifa ya maandishi kufika ofisi ya Chama ya Mkoa na Makao Makuu ataendelea kupata huduma kama ifuatavyo:-

(a) Endapo katika kipindi cha miezi sita Mwanachama husika ambaye ajira yake ilikoma na amefanikiwa kuajiriwa au kujiajiri na kuendelea kulipa ada zake kwa Chama ataendelea kupata huduma za uanachama.

(b) Endapo ajira imekoma kutokana na sababu za mgogoro wa kikazi ambao upo katika vyombo vya usimamizi wa haki na haujatolewa uamuzi ataendelea kuwa Mwanachama.

(c) Baada ya mgogoro kumalizika kwa Mwanachama kupata tuzo ya kurudishwa kazini au kulipwa haki zake atawajibika kulipa malimbikizo ya ada na kuendeleza uanachama wake.

## 9. UANACHAMA WA HESHIMA

(a) Wanachama ambao ni wastaafu wenye utumishi uliotukuka, waliojitolea kwa hali na mali kuwatumikia Wafanyakazi wanaweza kutunukiwa uanachama wa Heshima.

(b) Wanachama wa Heshima, watakuwa na haki za uanachama, isipokuwa haki za kuchagua, kuchaguliwa na kupiga kura kwenye vikao vya maamuzi.

(c) Mkutano Mkuu wa TUICO Taifa utapokea na kuteua majina ya wastaafu ambao watapendekezwa na Katibu Mkuu kutunukiwa uanachama wa heshima.

## 10. USHIRIKI WA WANACHAMA WA MAKUNDI MAALUMU KATIKA CHAMA

(a) Wafanyakazi ambao ni Wanachama wa makundi maalumu ya Wanawake, Vijana, Watu wenye Ulemavu, Wataalamu na Viongozi waandamizi sehemu za kazi, wana haki, fursa na wajibu sawa kwenye Chama na kushiriki shughuli za Chama kama Wanachama wengine.

(b) Chama kitaanzisha Kamati za Makundi Maalumu ili kuhakikisha wanapata haki zao za kikatiba, wanafaidi fursa zilizopo na wanatimiza wajibu wao kwa Chama.

## 11. OFISI ZA CHAMA

Chama kitakuwa na Ofisi kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi za Matawi mahali pa kazi ambapo kuna Wanachama kumi na kuendelea.

(b) Ofisi za Kanda na Mikoa kama itakavyoamriwa na Baraza Kuu kwa kuzingatia vigezo vya wingi wa shughuli za Chama, wingi wa Wanachama na uwezo wa kujiendesha kimapato.

(c) Ofisi ya Makao Makuu ya Chama ambayo itakuwa Dar es Salaam.

## 12. UTENDAJI WA OFISI

12.1 Ofisi za Chama zitaongozwa na Makatibu wafuatao:-

(i) Makatibu wa Matawi wataongoza Ofisi za TUICO sehemu za kazi.

(ii) Makatibu wa Mikoa wataongoza Ofisi za Mikoa.

(iii) Makatibu wa Kanda wataongoza Ofisi za Kanda.

(iv) Katibu Mkuu ataongoza Ofisi ya Makao Makuu.

12.2 Bila kuathiri utendaji wa Ofisi tajwa hapo juu, Ofisi zote zitawajibika kwa Katibu Mkuu wa Chama.

12.3 Utekelezaji wa shughuli za Chama katika ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa utasimamiwa na Kamati ya Utendaji ya ngazi husika. Utekelezaji wa shughuli za matawi utasimamiwa na Halmashauri za Matawi husika.

# 13. SEKTA, IDARA NA VITENGO

## 13.1 Sekta za Chama

Chama kina Sekta Kuu Nne (4) za kazi na shughuli zinazohusiana nazo kama ifuatavyo:-

(i) Sekta ya Viwanda.

(ii) Sekta ya Biashara.

(iii) Sekta ya Taasisi za Fedha.

(iv) Sekta ya Huduma na Ushauri.

## 13.2 Idara za Chama

Chama kitakuwa na Idara Nne (4) kama ifuatavyo:-

(i) Idara ya Elimu na Uimarishaji.

(ii) Idara ya Utumishi na Utawala.

(iii) Idara ya Uhasibu.

(iv) Idara ya Wanawake, Watu wenye Ulemavu, Afya na Usalama.

## 13.3 Vitengo vya Chama

Chama kitakuwa na Vitengo Vinne (4) kama ifuatavyo:-

(i) Kitengo cha Sheria.

(ii) Kitengo cha Uchumi na Takwimu.

(iii) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.

(iv) Kitengo cha Uhamasishaji, Uimarishaji na Vijana.

# 14. MATAWI, MIKOA, KANDA NA TAIFA

Kutakuwa na Matawi, Mikoa, Kanda na Taifa kama ifuatavyo:-

## 14.1 MATAWI YA CHAMA

Chama kitakuwa na matawi mahali pa kazi kama yatakavyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba , Kanuni na Sheria za Kazi.

## 14.2 WAWAKILISHI WA CHAMA SEHEMU ZA KAZI

Chama kitakuwa na Wawakilishi wake mahali pa kazi ambapo Wanachama wake wameajiriwa kama ifuatavyo:-

(a) Mahali pa kazi penye mwanachama mmoja mpaka wanachama tisa, mwakilishi mmoja, ambaye atawajibika kwa Katibu wa Mkoa kwa shughuli zote za Chama.

(b) Mahali pa kazi penye wanachama kumi mpaka wanachama ishirini; wawakilishi watatu, ambao ni Mwenyekiti wa Tawi, Katibu wa Tawi na angalau Mjumbe mmoja awe mwanamke miongoni mwa Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi.

(c) Mahali pa kazi penye wanachama ishirini na moja mpaka wanachama mia moja; wawakilishi kumi, ambao ni Mwenyekiti wa Tawi, Katibu wa Tawi na Wajumbe nane, angalau Wajumbe watatu wawe Wanawake miongoni mwa Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi.

(d) Mahali pa kazi penye wanachama zaidi ya mia moja; wawakilishi kumi na tano, ambao ni Mwenyekiti wa Tawi, Katibu wa Tawi na Wajumbe kumi na tatu, angalau Wajumbe watano wawe Wanawake miongoni mwa Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi.

## 14.3 MIKOA YA CHAMA

Mikoa ya Chama ni Ishirini na Mbili (22) ambayo ni:

1. Arusha
2. Dodoma
3. Ilala
4. Iringa
5. Kagera
6. Kigoma
7. Kilimanjaro
8. Kinondoni
9. Lindi
10. Mara
11. Mbeya
12. Morogoro
13. Mtwara
14. Mwanza
15. Pwani
16. Rukwa
17. Ruvuma
18. Shinyanga
19. Singida
20. Tabora
21. Tanga
22. Temeke

## 14.4 MADARAJA YA MIKOA

(a) Mikoa inaweza kugawanywa katika madaraja ya A, B na C kulingana na wingi wa wanachama, mapato ya Chama na utekelezaji wa shughuli za Chama katika mkoa husika.

(b) Kamati ya Utendaji ya Taifa inaweza kupandisha au kushusha daraja la Mkoa kwa kuzingatia shughuli za Chama kuongezeka au kupungua katika Mkoa husika.

## 14.5 KANDA ZA CHAMA

Kutakuwa na Kanda Nane (8) za Chama kama ifuatavyo:-

**(a) Kanda ya Dar es Salaam**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Ilala

ii. Kinondoni

iii. Temeke

**(b) Kanda ya Kaskazini**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Arusha

ii. Kilimanjaro

iii. Tanga

**(c) Kanda ya Kati**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Dodoma

ii. Singida

**(d) Kanda ya Kusini**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Ruvuma

ii. Mtwara

iii. Lindi

**(e) Kanda ya Magharibi**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Tabora

ii. Kigoma

**(f) Kanda ya Mashariki**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Morogoro

ii. Pwani

**(g) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Iringa

ii. Mbeya

iii. Rukwa

**(h) Kanda ya Ziwa**

Mikoa katika Kanda hii ni:-

i. Mara

ii. Kagera

iii. Shinyanga

iv. Mwanza

## 15. VIKAO VYA CHAMA

### (a) Madaraka

Vikao vya Chama kwa ngazi za Matawi, Mikoa, Kanda hadi Taifa vitafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Chama. Vikao vya juu vitakasimu madaraka yake kwa vikao vya ngazi ya chini yake itokeapo sababu maalumu kwa utaratibu utakaofaa.

### (b) Taratibu za Vikao vya Chama

Vikao vya Chama vya ngazi za chini vitatoa ushauri na mapendekezo kwa vikao vya ngazi za juu. Vikao vya Chama vya ngazi za juu vitatoa ushauri, uamuzi na maelekezo kwa ngazi za chini kulingana na madaraka ya Kikatiba.

## 16. UENDESHAJI WA VIKAO VYA CHAMA

(a) Akidi ya Wajumbe katika Vikao na Mikutano yote ya Chama itakuwa si chini ya nusu (1/2) ya Wajumbe halali wa Vikao na Mikutano husika.

(b) Wajumbe wa kila Kikao/Mkutano watakuwa na haki ya kushiriki katika majadiliano ya agenda zinazojadiliwa wakiongozwa na Mwenyekiti.

(c) Uamuzi wa mjadala wa agenda zinazojadiliwa kwenye Kikao/Mkutano utafikiwa kwa makubaliano ya Wajumbe wengi.

(d) Iwapo muafaka hautafikiwa kwenye mjadala, uamuzi utafikiwa kwa kupiga kura ya siri. Endapo kura

zitalingana Mwenyekiti wa Kikao/Mkutano husika atapiga kura ya nyongeza.

(e) Uamuzi kwa Agenda zifuatazo utafikiwa kwa kura za siri:-

i. Uchaguzi.

ii. Migomo.

iii. Kuvunja Chama.

iv. Kuunganisha Vyama.

v. Kura ya kutokuwa na imani na uongozi/kiongozi wa Chama.

Uamuzi wa kura za siri utazingatia matakwa ya Katiba ya Chama na Sheria husika.

(f) Katibu Msaidizi au Mtendaji wa Chama atakayepewa dhamana ya kukaimu cheo cha Katibu wa Mkoa, Kanda au Mkuu wa Sekta atakuwa na haki ya kuwa mjumbe katika vikao vya Kikatiba vya Chama.

(g) Kusitishwa kwa haki ya kupiga na kupigiwa kura kutatokana na kukiukwa kwa Katiba ya Chama na Kanuni zake.

(h) Agenda rasmi za Kikao/Mkutano ni zile zitakazowasilishwa na Katibu wa Kikao husika.

## 17. UCHAGUZI MKUU WA CHAMA

Itakapofika wakati wa Uchaguzi Mkuu, Wajumbe wa Baraza Kuu wataidhinisha ratiba ya uchaguzi kama

itakavyowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa. Mara baada ya ratiba hiyo kuidhinishwa, Sekretarieti ya Chama itaanza maandalizi ya utekelezaji wa ratiba ya uchaguzi chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu.

## 18. KUGOMBEA UONGOZI KATIKA CHAMA NA SIFA ZAKE

(a) Viongozi wa Chama watapatikana kwa taratibu za uchaguzi. Taratibu hizi zitaongozwa na Katiba, Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Chama. Nafasi zote za kuchaguliwa zitatangazwa wazi, na waombaji wa nafasi hizo wataomba katika ngazi zinazohusika kwa kujaza fomu maalum.

(b) Nafasi za uongozi wa Chama zitagombewa na mfanyakazi ambaye ni Mwanachama hai wa Chama mwenye sifa za kugombea uongozi kama zilivyoainishwa katika Masharti, Kanuni na Taratibu za uchaguzi wa TUICO. Utaratibu huu wa kugombea uongozi pia utatumika kwenye Kamati za Makundi Maalumu.

(c) Chama kinaweza kuanzisha Kamati za Makundi Maalumu ya Wanachama ndani ya Chama kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

(d) Kamati za Makundi Maalumu ya Wanachama ambazo kutokana na mazingira na mahitaji ya Chama zinazoweza kuanzishwa ni pamoja na:-

(i) Kamati za Wanawake.

(ii) Kamati za Vijana.

(iii) Kamati za Wataalamu na Viongozi Waandamizi.

(iv) Kamati za Wafanyakazi wenye Ulemavu.

(e) Baraza Kuu litakapoanzisha Kamati za Makundi Maalumu ya Wanachama ndani ya Chama, pia litapitisha miongozo ya miundo, majukumu, usimamizi na masuala yote yanayohusiana na Kamati hizo.

(f) Viongozi wa Kamati za Makundi Maalumu ya Wanachama, Wadhamini wa Chama na Viongozi wengine wote wa Chama wa kuchaguliwa au kuteuliwa watakuwa madarakani kwa kipindi kisichozidi miaka mitano (5). Kwa viongozi waliochaguliwa ili kujaza nafasi zilizo wazi za uongozi ndani ya Chama kwa ngazi husika watakuwa madarakani kwa kipindi cha uongozi kilichobakia.

## 19. VIONGOZI NA WATENDAJI WA CHAMA

(a) Viongozi na Watendaji wa Chama watachaguliwa, kuteuliwa, kuajiriwa, kusimamishwa au kuachishwa na mamlaka husika kwa mujibu wa Katiba ya Chama na Kanuni za Utumishi za TUICO.

(b) Mwanachama yeyote ambaye ameajiriwa au kuteuliwa kuwa Mtendaji ndani ya Chama, uanachama wake utaendelea kutambuliwa.

## 20. KUSIMAMISHWA KWA MUDA, HAKI YA KUPIGA NA KUPIGIWA KURA

(i) Mwanachama yeyote ambaye hajalipa michango yake kamili kwa zaidi ya miezi sita (6) hatakuwa na

haki ya kupiga wala kupigiwa kura katika vikao vya Chama hadi hapo atakapolipa malimbikizo ya ada anazodaiwa.

(ii) Mwanachama yeyote aliyehukumiwa kwa kosa la jinai hatakuwa na haki ya kupiga wala kupigiwa kura katika vikao vya Chama hadi hapo Kamati ya Utendaji ya Taifa itakapoamua vinginevyo.

## 21. WAJUMBE WA MIKUTANO MIKUU YA UCHAGUZI WANAOMALIZA MUDA WAO WA UONGOZI

(a) Wakati wa Uchaguzi Mkuu ngazi ya Tawi Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi watajiuzulu nyadhifa zao kupisha uchaguzi kufanyika.

(b) Wakati wa Uchaguzi Mkuu ngazi ya Mkoa, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda kutoka Mkoa huo, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa wanaomaliza muda wao wa uongozi kabla ya kuanza zoezi la uchaguzi watajiuzulu nyadhifa zao kupisha Uchaguzi kufanyika isipokuwa Katibu wa Mkoa.

(c) Wakati wa Uchaguzi Mkuu ngazi ya Kanda, Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Kanda pamoja na Mwenyekiti wa Kanda wanaomaliza muda wao wa uongozi kabla ya kuanza zoezi la uchaguzi watajiuzulu nyadhifa zao kupisha uchaguzi kufanyika isipokuwa Katibu wa Kanda.

(d) Wakati waUchaguzi Mkuu ngazi ya Taifa Wajumbe wa kuchaguliwa wa Baraza Kuu, Katibu Mkuu na Mwenyekiti wa Taifa wanaomaliza muda wao kabla ya kuanza zoezi la uchaguzi watajiuzulu nyadhifa zao kupisha uchaguzi kufanyika.

(e) Bila kuathiri kifungu (d) hapo juu, Katibu Mkuu Msaidizi, Wakuu wa Sekta, Makatibu wa Kanda na Makatibu wa Mikoa wataendelea kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi kutokana na nyadhifa zao.

## 22. MAANDALIZI NA USIMAMIZI WA UCHAGUZI

### (a) MAANDALIZI

i. Kutaundwa Kamati ya Maandalizi ya Uchaguzi katika ngazi husika itakayopitia na kuhakiki sifa za wagombea na usahihi wa ujazaji wa fomu za wagombea zilizorejeshwa katika ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa.

ii. Wajumbe wa Kamati za Maandalizi ya Uchaguzi watateuliwa na Kamati za Utendaji katika ngazi husika. Kamati itakuwa na wajumbe watano akiwemo Katibu wa Chama wa ngazi husika.

iii. Kamati hii itatoa mrejesho kwa mgombea ambaye fomu yake ina dosari isiyokidhi masharti ya uchaguzi kupitia Katibu wa Chama wa ngazi husika katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne tangu tarehe ya mwisho ya kurejeshwa kwa fomu.

iv. Bila kuathiri maelezo ya Kanuni ya (i) na (ii) hapo juu, Katibu wa Mkoa atakuwa ndiye mhakiki wa fomu zote za wagombea ngazi ya Tawi.

v. Wagombea wa uongozi katika ngazi zote hawatakuwa na sifa ya kuwa wajumbe wa Kamati za Maandalizi za Uchaguzi.

### (b) USIMAMIZI WA UCHAGUZI

i. Wakati wa Uchaguzi wa Chama ngazi ya Tawi hadi Taifa, kutaundwa Kamati za Usimamizi za Uchaguzi kwa ngazi husika.

ii. Kamati ya Usimamizi itakuwa na Mwenyekiti wa Muda na Wajumbe wengine wawili.

iii. Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi ambaye ni Katibu wa Chama wa ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa atasaidiana na Kamati hii katika kufanikisha Uchaguzi.

iv. Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi ngazi ya Tawi ni Katibu wa Mkoa.

## 23. MGOMBEA WA NAFASI YA KATIBU MKUU WA CHAMA

(a) Mgombea nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama, ambaye ndiye Mtendaji na Msemaji Mkuu wa Chama ni lazima awe na sifa za kugombea uongozi huo kama ilivyofafanuliwa kwenye Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Chama.

(b) Pamoja na mgombea kutimiza sifa hizo, Mwanachama anayegombea nafasi ya Katibu Mkuu ni lazima awe na

uzoefu wa shughuli za Chama, busara na uwajibikaji. Kigezo cha miaka ya kustaafu kazi kwa umri, si cha lazima kwa mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama.

(c) Iwapo Mwanachama amechaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama atalazimika kuacha kazi kutoka kwenye ajira yake ya awali mara anapochaguliwa kushika madaraka hayo kwenye Chama.

## 24. MATUKIO YASIYOTARAJIWA KABLA YA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA

Endapo itatokea wagombea uongozi katika Chama wa ngazi husika watafariki kabla ya uchaguzi na kusababisha nafasi husika kukosa wagombea, wakati ambapo kabla ya kutokewa na hali hiyo tayari wagombea walikwishathibitishwa ugombea wao, Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa ngazi husika utaahirishwa kwa muda wa siku thelathini (30) ili kutoa nafasi kwa Wanachama wengine kujitokeza kuomba uongozi kwa nafasi za:-

(a) Katibu wa Tawi.

(b) Mwenyekiti wa Tawi.

(c) Mwenyekiti wa Mkoa.

(d) Mwenyekiti wa Kanda.

(e) Mwenyekiti wa Taifa.

(f) Katibu Mkuu.

(g) Wenyeviti wa Kamati za Makundi Maalumu.

## 25. KUJAZA NAFASI ZA UONGOZI ZILIZO WAZI

Kila nafasi itakapoachwa wazi katika uongozi wa Chama ikiwa ni pamoja na kiongozi kushindwa kutumikia nafasi yake ya uongozi kwa zaidi ya mwaka mmoja, Kikao kinachohusika kitaijaza nafasi hiyo mapema iwezekanavyo, kwa mujibu wa Katiba, Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa TUICO kama ifuatavyo:-

### (a) Nafasi ya Halmashauri ya Tawi

Endapo nafasi ya Mwenyekiti na Katibu itakuwa wazi au Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi watapungua chini ya nusu ya Wajumbe halali Uchaguzi wa kujaza nafasi husika utafanyika mapema iwezekanavyo.

### (b) Nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa

Bila kuathiri yaliyoelekezwa hapo juu, Kikao cha Uchaguzi cha kumchagua Mwanachama wa kujaza nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa, ni Kamati ya Utendaji ya Mkoa husika. Wanachama wanaostahili kugombea nafasi hii, ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa husika.

### (c) Nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa

Endapo nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa kutoka Sekta husika zitakuwa wazi kwa sababu yoyote ile katika kipindi cha uongozi, nafasi hizo zitajazwa kwa taratibu za uchaguzi wa Chama, katika Kikao Maalumu cha uchaguzi. Wanachama wanaostahili kugombea nafasi hizo ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka Sekta husika.

Kikao maalumu cha uchaguzi kitakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Mkoa.

(ii) Katibu wa Mkoa.

(iii) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa wa Sekta zilizobakia.

(iv) Wawakilishi wa Chama (Union Representatives) kutoka Sekta husika mahali pa kazi penye Wanachama sita hadi tisa (6 hadi 9).

(v) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa wa Sekta husika.

(vi) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Mkoa.

## (d) Nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda

Nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda itakapokuwa wazi itajazwa na Mkutano Mkuu wa Kanda. Wanachama wanaostahili kugombea nafasi hiyo ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda hiyo, ili kumalizia kipindi cha uongozi kilichobaki.

## (e) Nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji Kanda

Endapo nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kanda zitakuwa wazi kwa sababu yoyote katika kipindi cha uongozi, Kikao cha Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda wa Sekta husika utafanya uchaguzi wa kujaza nafasi iliyo wazi. Wanachama wanaostahili kugombea nafasi hizo watatoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda kutoka Sekta husika.

### (f) Nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa

Endapo nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa zitakuwa wazi kwa sababu yoyote katika kipindi cha uongozi, Kikao cha Baraza Kuu kitafanya uchaguzi wa kujaza nafasi hizo. Wanachama wanaostahili kugombea nafasi hizo watatoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka Sekta husika.

## 26. NAFASI ZA KUTEULIWA KATIKA CHAMA

Mapendekezo ya majina kwa nafasi zote za kuteuliwa yatapelekwa na Katibu Mkuu wa Chama kwenye Mamlaka za uteuzi.

## 27. WAALIKWA KWENYE VIKAO VYA BARAZA KUU

(a) Wawakilishi wa Chama kwenye Baraza Kuu la Shirikisho, Wadhamini wa Chama Taifa, Mwakilishi kwenye Kamati ya Utendaji ya Shirikisho wataalikwa kuhudhuria vikao vya Baraza Kuu la TUICO isipokuwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura katika vikao hivyo. Kutokana na idadi ya Wawakilishi kwenye Baraza Kuu la Shirikisho kuwa kubwa, kutakuwa na utaratibu maalumu wa kupanga makundi ya Wajumbe watakaohudhuria.

(b) Katibu Mkuu kwa kushauriana na Sekretarieti anaweza kumualika Mshiriki yeyote kama itakavyoonekana inafaa.

## 28. MAPATO YA CHAMA

### (a) ADA YA WANACHAMA

(i) Ada za kila mwezi zitaamuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa. Kiwango cha Ada ya Mwanachama kila mwezi kitakuwa asilimia mbili (2%) ya mshahara wa Mwanachama au kama itakavyopangwa vinginevyo na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(ii) Kwa Wanachama wanaojitegemea wenyewe/ waliojiajiri, kiwango chao cha Ada ya Mwanachama hakitapungua asilimia mbili ya Kima cha chini cha mshahara cha wakati huo kwa Sekta husika.

(iii) Chama kitarejesha/kubakiza asilimia nne (4%) ya ada za wanachama Tawini kwa kila mwezi. Fedha hizo zitatunzwa kwenye Akaunti ya Tawi itakayofunguliwa na kuhakikiwa na Ofisi ya Katibu wa Mkoa husika. Fedha hizo zitatumika kwa maendeleo ya Chama Tawini.

### (b) ADA YA UWAKALA (AGENCY SHOP FEE)

Ada hii italipwa kwa kiwango sawa cha Ada anayolipa Mwanachama na itasimamiwa na Katibu Mkuu kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na6 ya mwaka 2004, Kanuni (GN 42 ya mwaka 2007) na Taratibu za Chama.

### (c) MICHANGO

Kila itakapohitajika, wanachama watawajibika kutoa michango itakayopangwa na Kamati ya Utendaji ya

Taifa katika masuala yanayohusiana na migogoro, maendeleo ya Wafanyakazi na Chama chenyewe.

## 29. FEDHA NA MALI ZA CHAMA

(a) Chama kitapokea fedha na kutoa Stakabadhi maalumu ya Chama na kuhifadhi fedha hizo kwenye Akaunti ya Chama.

(b) Malipo ya fedha yatafanyika kulingana na maelekezo ya Baraza Kuu, kama yatakavyokuwa katika Taratibu za Chama na Kanuni za Fedha.

(c) Chama kinaweza kununua Mali inayohamishika/isiyohamishika kwa idhini ya Baraza Kuu na kuwa chini ya udhamini wa Bodi ya Wadhamini. Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki Katibu Mkuu anaweza kununua mali ya Chama inayohamishika/isiyohamishika na kuitolea taarifa katika Baraza Kuu.

(d) Chama kinaweza kuwekeza fedha zake katika miradi ya uzalishaji, ununuzi wa hisa kwa kuzingatia Sera ya Chama ya Uwekezaji kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu.

## 30. MALIPO YA VIONGOZI NA WATENDAJI

Viongozi na Watendaji wa Chama watalipwa posho na stahili nyingine kulingana na maamuzi ya Baraza Kuu.

## 31. MFUKO MAALUMU WA AKIBA/MGOMO

(a) Chama kinaweza kuanzisha Mfuko Maalumu wa Akiba/Mgomo ambao utatunzwa na Chama kwa

madhumuni ya kufanikisha shughuli za Chama kwa manufaa ya Wanachama.

(b) Mfuko huo utaendelezwa kwa kuchangiwa na Chama, Wanachama na vyanzo vingine kama itakavyokubaliwa na Baraza Kuu la Chama.

(c) Baraza Kuu litaandaa Sera, Taratibu za Uendeshaji na Usimamizi wa Mfuko huo, ikiwa ni pamoja na kuweka viwango vya kuchangia, kuweka kinga ya fedha za mfuko na namna ya Chama na Wanachama watakavyonufaika.

## 32. UWEZO WA CHAMA KUKOPA

(a) Chama kina fursa ya kukopa fedha kutoka Benki au Taasisi nyingine zinazotoa mikopo ili kukiwezesha kuanzisha, kuwekeza na kuendeleza miradi yenye lengo la kuboresha uwezo wake.

(b) Baraza Kuu litapitisha Sera ya Uwekezaji itakayoongoza taratibu za Chama kukopa, kuanzisha miradi ya kiuchumi na uwekezaji.

## 33. USIMAMIZI WA FEDHA ZA CHAMA TAWINI

Mapato ya Chama katika ngazi ya Tawi yatasimamiwa kwa utaratibu ufuatao:

(a) Kufungua Akaunti Benki kwa jina la Tawi la TUICO mahala pa kazi husika.

(b) Kuwepo kwa watia saini katika Akaunti ya Tawi watakaochaguliwa miongoni mwa Wajumbe wa

Halmashauri ya Tawi chini ya usimamizi wa Katibu wa Mkoa.

(c) Matumizi ya mapato ya Tawi yatakuwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Chama Tawini.

(d) Malipo yoyote yatokanayo na mapato ya Tawi yaandaliwe na kuidhinishwa na Halmashauri ya Tawi.

(e) Taarifa za mapato na matumizi zitayarishwe na Katibu wa Tawi, zitunzwe na kuwasilishwa kwenye vikao vya Halmashauri ya Tawi, Mkutano wa Wanachama na nakala kwa Katibu wa Mkoa.

## 34. UKAGUZI WA FEDHA, MALI NA DAFTARI LA WANACHAMA

(a) Hesabu na mali za Chama zitakaguliwa mara moja kwa mwaka wa fedha na Mkaguzi wa Nje wa Hesabu aliyesajiliwa ambaye atateuliwa na Baraza Kuu.

(b) Taarifa ya Ukaguzi wa Fedha itapelekwa Baraza Kuu na kwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya 2004, Kifungu cha 51.

(c) Mwanachama akiomba taarifa za fedha na mali za Chama atapewa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Chama.

(d) Mwanachama atakayehitaji kuona vitabu na Orodha ya Wanachama, atakuwa na haki ya kufanya hivyo baada ya kumuandikia barua Katibu wa Chama wa ngazi husika akitaja sababu za kufanya hivyo.

## 35. USHIRIKIANO NA ASASI ZA KIJAMII

Bila kuathiri yaliyomo katika Katiba, Chama kitakuwa na mahusiano mazuri na Asasi za Kijamii za kitaifa na kimataifa ambazo zina malengo na mwelekeo wa kusaidia Wafanyakazi na Vyama vya Wafanyakazi.

## 36. KUVUNJWA AU KUUNGANISHWA VYAMA

(a) Chama kinaweza kuacha kufanya shughuli zake na kuvunjwa kama pendekezo litapitishwa kwa theluthi mbili (2/3) ya Wanachama wote na mali zote zitakabidhiwa kwa Wadhamini wa TUICO Taifa kwa hifadhi.

(b) Chama kinaweza kuamua kuvunjwa baada ya uamuzi wa kutaka kuungana na Chama kingine. Uamuzi wa kuungana na Chama kingine utaamuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa. Uamuzi huo utaamuliwa kwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

(c) Iwapo Chama kitavunjwa na kuungana na Chama kingine mali na madeni ya Chama yatachukuliwa na Chama kipya.

## 37. MGOGORO KATI YA TUICO NA CHAMA SHIRIKI CHA SHIRIKISHO

Mgogoro wowote kati ya TUICO na Chama Shiriki cha Shirikisho, lazima uwasilishwe kwenye vikao vya Kamati ya Utendaji TUICO Taifa na Baraza Kuu TUICO kwa kujadiliwa na kutolewa maelekezo.

## 38. UTUMISHI NDANI YA CHAMA

Chama kitaajiri Watumishi wa Chama kulingana na mahitaji na maelekezo ya Muundo na Kanuni za Utumishi za Chama. Watumishi watalipwa mishahara na posho kulingana na Kanuni za Utumishi, Muundo wa Utumishi, Mkataba wa Hali Bora na Nyaraka zilizopitishwa na Baraza Kuu.

## 39. SEKRETARIETI YA CHAMA

Kutakuwa na Sekretarieti ya Chama Makao Makuu, ambayo itaundwa na Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Wakuu wa Sekta, Idara na Vitengo kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Chama.

## 40. AJIRA ZA MIKATABA YA MUDA MAALUMU

(a) Iwapo itatokea haja ya kuwa na Ajira za Mikataba ya Muda Maalumu, Chama kinaweza kuajiri Mfanyakazi kwa Ajira ya Mkataba wa Muda Maalumu.

(b) Mfanyakazi wa TUICO ambaye ajira yake itakoma kwa sababu ya kustaafu kwa lazima kutokana na umri, anaweza kuajiriwa kwa ajira ya Mkataba wa Muda Maalumu kwa maombi ya maandishi. Sifa na vigezo vya kuajiriwa kwa Mkataba wa Muda Maalumu ni mahitaji ya Chama, Uwezo, ujuzi na utayari wa mwombaji kuendelea kukitumikia Chama kwa ufanisi.

(c) Kanuni za Utumishi zitafafanua namna Chama kitakavyoshughulikia ajira za Mikataba ya Muda Maalumu.

## 41. MIIKO, MAADILI NA MAMLAKA YA UDHIBITI

### (a) Miiko

#### (i) Miiko ya Viongozi wa TUICO

Viongozi wa Chama hawaruhusiwi kuwa na wadhifa katika Chama cha Siasa au Serikali ambao unaweza kuzua mgogoro wa kimaslahi. Ngazi za uongozi kwenye Vyama vya Siasa ni kuanzia Jimbo, na kuendelea. Kwa upande wa Serikali ni kuanzia Wilaya na kuendelea.

#### (ii) Miiko ya Watendaji

Watendaji wote wa Chama watajitolea kukitumikia Chama na hawatajihusisha katika madaraka mengine ya kiutendaji nje ya Chama bila ya ridhaa ya Kamati ya Utendaji TUICO Taifa. Nafasi hiyo iwe ya kuchaguliwa, kuteuliwa au kuajiriwa.

#### (iii) Miiko ya Wanachama

Mwanachama yeyote haruhusiwi kusimamisha uchaguzi Mahakamani au kupeleka Mahakamani malalamiko au rufaa inayohusiana na uchaguzi wa Viongozi wa Chama au utekelezaji wa Katiba, Kanuni za Chama, Masharti, Kanuni au Taratibu za Uchaguzi kabla ya hatua zote za kushughulikia malalamiko ya rufaa ndani ya Chama kukamilika. Mwanachama atakayekiuka miiko hii atasimamishwa uanachama wake mara moja.

### (b) Maadili

Maadili ya Viongozi, Watendaji na Wanachama wa TUICO ni:-

(i) Kulinda na kutetea Katiba na Kanuni za Chama.

(ii) Kuunga mkono kwa kauli na vitendo, juhudi za kuendeleza Chama.

(iii) Kuwa muwazi, mkweli, mwaminifu na mwadilifu.

(iv) Kuheshimu maamuzi na kutunza siri za Vikao na Mikutano kama inavyoelekezwa na Katiba na Kanuni za Chama.

### (c) Mamlaka ya Udhibiti Miiko na Maadili ya Chama

Kamati ya Utendaji ya Taifa ndiyo Chombo chenye Mamlaka ya kusimamisha Uanachama na kudhibiti Miiko na Maadili ya Wanachama na Viongozi kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

## 42. WASHAURI WA CHAMA

(a) Chama kitakuwa na Washauri ambao walikuwa watendaji/Viongozi waliotumikia Chama ngazi ya Taifa, wenye uzoefu, maarifa na weledi katika uendeshaji wa Vyama vya Wafanyakazi.

(b) Mshauri/Washauri waChama watapewa Uanachama wa Heshima na watakuwa na jukumu la kushauri kuhusu uendeshaji wa shughuli za Chama kulingana na misingi mikuu ya Chama, utamaduni na madhumuni ya Chama.

(c) Baraza Kuu litapokea na kupitisha jina/majina ya washauri hao kama yatakavyowasilishwa na Katibu Mkuu kwa kushauriana na Mwenyekiti wa TUICO Taifa.

## 43. WAHAMASISHAJI WA CHAMA (ACTIVISTS)

(a) Chama kitawatambua na kuwatumia wahamasishaji Katika kufanikisha shughuli za ujenzi wa Chama. Wahamasishaji (Activists) watasaidia utekelezaji wa shughuli zinazotokana na Misingi Mikuu ya Chama.

(b) Chama kitakuwa na jukumu la kuwapa mafunzo Wahamasishaji ili kufanikisha majukumu yao na kuratibu utekelezaji wa shughuli ambazo zitafanywa na wahamasishaji hao.

## 44. MAJADILIANO NA MIGOGORO YA KIKAZI

Migogoro inayotokana na Majadiliano ya Pamoja na kusababisha migomo, Kamati ya Utendaji ya Taifa itatoa idhini kwa Katibu Mkuu kushughulikia.

## 45. MGONGANO WA TAFSIRI NA MATUMIZI YA KANUNI HIZI

Mgongano wa Tafsiri na matumizi ya Kanuni hizi utakaojitokeza utapelekwa Ofisi ya Katibu Mkuu na hatimaye kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa kwa ufafanuzi.

## 46. UTARATIBU WA HATI YA IDHINI (PROXY)

(a) Utaratibu wa kawaida kwa maamuzi ya shughuli za Chama, hujadiliwa na kupitishwa na Mamlaka ya Kikao husika. Wakati mwingine hutokea mazingira ambayo shughuli ya Chama ya Kikao husika inahitaji utekelezaji wa haraka ambao hauwezi kusubiri kuitishwa kwa Kikao husika ili kushughulikiwa.

(b) Bila kuathiri matakwa ya Katiba ya Chama, endapo mazingira kama hayo hapo juu yatatokea, Katibu Mkuu anaweza kutumia utaratibu wa Hati ya Idhini (Proxy) ili kushughulikia jambo hilo au kuitisha kikao kitakachoshughulikia suala hilo katika mazingira hayo.

(c) Taarifa ya ushughulikiaji wa jambo hilo, lazima iandaliwe na kuwasilishwa kwenye Kikao husika.

## 47. MAREKEBISHO YA KANUNI ZA CHAMA

Kanuni hizi zinaweza kurekebishwa/kubadilishwa kwa kufuata Taratibu, Kanuni na Katiba ya Chama wakati wowote pale itakapotokea haja ya kufanya hivyo Kisheria au Kikatiba ili ziendane na mahitaji ya wakati huo.

S.L.P. 5680, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: (0) 22 2866910 / 2866960 | Nukushi +255 (0) 22 2866911
Barua pepe: tuico2004@yahoo.com | Tovuti: www.tuico.or.tz